بسم الله الرحمن الرحيم

UTANGULIZI

Sifa njema zinamstahiki Allah mtukufu, na swala na salam zimfikie mtume wetu Muhammad na jamaa zake na maswahaba wake wote.

Baada ya hayo:

Hii ni tafsiri ya ufupisho wa muhadhara alioutoa sheikh Abdullah Abdurrahim Albukhary Allah amhifadhi na kuupa jina: ni upi usalaf?

Nimeonelea kutafsiri muhadhara huo kwa sababu zifuatazo:

1.kutokana na faida nyingi zilizoelezwa katika muhadhara huo.

2.kuwaelemisha watu wasiojua usalaf

3.kuwazindusha walioghafilika na manhaj hii ya mtume ﷺna maswahaba wake.

4.kujaribu kuieneza daa'wa salafiyya kwa njia hii ya maandishi.

5.kutaka radhi za Allah mtukufu

Ninamuuomba Allah mtukufu kwa majina yake mazuri na sifa zake tukufu akijaalie kitabu hiki kidogo ni chenye kutakaswa kwa ajili ya uso wake mtukufu ,pia ninamuomba Allah amlipe kheri sheikh Abdallah Al bukhary,na kila aliefanikisha kuitoa tafsiri hii wakiwemo wachapishaji na kila atakae kisoma na kuyafuata yote yaliyomo katika kitabu hiki.

Abu Hashim Abdulkadir Bin Hashim Al–Musawaa

8/8/2017 **15/11/ 1438**

NUKTA YA KWANZA

KUWEKA WAZI MAANA YA USALAF KATIKA LUGHA

Siin, Lam na Faa ni asili inayofahamisha kutangulia,kwa hiyo tamshi la salaf katika lugha linamaanisha mwenye kutangulia.

Na huitwa hivyo salaf kila mwenye kukutangulia katika ndugu na mfano wake.

Na ni katika hayo maneno ya Allah mtukufu:

﴿ فَجَعَلْنَٰهُمْ سَلَفاً وَمَثَلاً لِّلاٰخِرِينَ ﴾

(Tukawafanya ni wenye kutangulia na mfano kwa waliokuja mwisho) (Surat Az-Zukhruf: 56)

Amesema imam albukhary Allah amrehemu katika tafsiri yake ya ayah hii: salaf ni waliotangulia katika wazee, tukawafanya ni wenye kutangulia ili wa mwisho wapate mawaidha kwa sababu yao.

Na ni katika hayo maneno ya Allah mtukufu :

﴿ وَأَن تَجْمَعُواْ بَيْنَ الأُخْتَيْنِ إِلاَّ مَا قَدْ سَلَفَ ﴾

(Na haram kukusanya baina ya dada wawili (kuwaoa) isipokua yaliyopita) (Surat An-Nisa':23)

Maana vitendo vyenu vilivyo pita, hilo ni lenye kuwekwa mbali, kuondolewa dhambi sio kuwa kitendo hicho kinafaa, kwa hiyo husemwa Fulani ana salaf watukufu, yaani ana wazee waliotangulia, amesema Arraaghib al-asfahaaniy Allah amrehemu katika (almufradat)

Alhafidh ibnul athiir na ibnu mandhur wanasema: salaf: ni mwenye kutangulia kwa umri na fadhla tu.

Ibnu mandhur Allah amrehemu anasema: Na salaf pia: ni mwenye kukutangulia katika wazee na jamaa wako waliojuu yako kwa umri na fadhla kwa hiyo lile kundi la kwanza katika taabiin limeitwa (assalafuswalih)

Na katika hadithi inayo fahamisha maana hiyo ni hadithi iliyokuja katika vitabu viwili sahihi kwa hadithi ya Aisha رضي الله عنها na hadithi ina kisa hiki:

Mtume ﷺalimnong'oneza binti yake fatma رضي الله عنها akalia, alipoona huzuni yake akamnong'oneza mara nyengine fatma رضي الله عنها akacheka, Aisha رضي الله عنها akamuuliza Fatma hakumuelezea.

Alipokufa mtume ﷺ Aisha رضي الله عنها alimuuza mara nyengine ndipo Fatma alipojibu kwa kusema :ama aliponinong'oneza mara ya kwanza ;alinielezea kuwa jibril alikua akimdhirishia quran mara moja kwa mwaka, na kuwa alimdhirishia hivi sasa mara mbili ,na akamwambia ;mimi sioni muda wangu na kifo isipokua umekaribia ,hivyo mche Allah na subiri ,kwani bora ya waliokutangulia ni mimi)

Fatma akasema nikalia kilio ulichokiona, alipoona huzuni yangu alininong'oneza mara ya pili ,akasema :ewe Fatma hivi huridhii kuwa wewe ni bibi mkubwa wa wanawake waumini,au bibi mkubwa wa wanawake wa umma huu?nikacheka kicheko kile ulichokiona)

Amesema Alhafidh Annawawy Allah amrehemu katika (sharhi ya swahih muslim)aliposherehesha maneno ya Mtume ﷺ

فانه نعم السلف انا لك

(kwani bora ya wenye kukutangulia ni mimi)akasema ;assalaf:ni mwenye kukutangulia , na maana yake :mimi ni mwenye kutangulia mbele yako

Hii ndio maana ya kilugha

NUKTA YA PILI

NI KINA NANI SALAF KATIKA ISTILAHI?

Imeshapita kuwa salaf katika lugha :ni waliokutangulia kwa umri na fadhla,sasa tunataja maana ya tamshi hili kwa istilahi.

Allah mtukufu amesema katika kitabu chake kitukufu

﴿وَالسَّبِقُونَ الأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَـجِرِينَ وَالأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُواْ عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الأَنْهَرُ خَـلِدِينَ فِيهَآ أَبَداً ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴾

(na waliotangalia wa mwanzo katika muhajirin na answar na wenye kuwafuatia wao kwa wema Allah amewaridhia na wao wakamridhia na amewaandalia pepo ambazo mito hupita mbele yake huko ndiko kufuzu kukubwa) (Surat At-Tawbah:100)

Na katika vitabu viwili swahihi kutokana na ibni Masuud رضى الله عنه amesema: amesema Mtume ﷺ

(خير الناس قرنى ثم الذين يلونهم , ثم الذين يلونهم,ثم يجئ أقوام تسبق شهادة أحدهم يمينه, ويمينه شهادته)(البخاري)

(bora ya watu ni karne yangu, kisha wanaowafuatia hao, kisha wanaowafuatia hao,kisha watakuja watu ambao ushahidi wa mmoja wao hutangulia kiapo chake,na kiapo chake hutangulia ushahidi wake)Bukhary

Na katika swahih muslim kutokana na Aisha رضى الله عنها anasema : mtu mmoja alimuuliza mtume ﷺni watu gani bora ? Akasema : ni karne ile ambayo mimi nipo, kisha ya pili, kisha ya tatu,

Na zipo hadithi nyengine nyingi zinazoelezea hivyo, aya iliyopita ya surati ttawba na hadithi zinafahamisha ubora wa maswahaba رضى الله عنهم na kuwa wao ndio watu bora wa umma huu baada ya mtume wa Allah ﷺ

Na bila shaka wao ni wenye kututangulia katika fadhla, ilmu na Imani رضى الله عنهم

Je kila mtu aliyeishi katika zama hizo zilizobarikiwa inatosha kuwa mtu huyo ni katika watu wema wanaofwatwa?

Hapana sio hivyo ,kwani kutangulia kwa zama hizo hakutoshi kubainisha hao salaf, ni lazima kuongezea sharti muhimu ambalo ni kuwafiki Qurani na hadithi na ufahamu wa maswahaba رضي الله عنهم ndio maana tunapata maimamu wa sunna wanaiwekea sharti istilahi hii, na kusema watu wema waliotangulia, ili watoke watu waovu waliotangulia katika baadhi ya waliokuwepo katika zama zao na wasiwe juu ya ufahamu wao na mfumo wao.

Ushahidi wa hilo ni Alqadariyya waliojitokeza baina ya kundi la maswahaba ,na hadithi ya Abdullahi bni Umar رضي الله عنهم ya kuwa ameepukana na hao Qadariyya ni hadithi mashuhuri na ni hadithi ya kwanza katika swahih muslim

Pia khawaarij waliotoka katika twaa ya Aliyرضي الله عنه na wengine katika maswahaba ,nao makhawaarij walikuwa baina ya maswahaba ,Ibni Abbas رضي الله عنه alipowajadili makhawaarij mjadala mashuhuri alioutoa Alhakim katika almustadrak kwa isnad sahihi . Na katika maneno aliyowaambia kuwa ni dalili ya upotevu wao;

(وانظروا ليس فيكم منهم اي من الصحابة)

(angalieni hakuna swahaba yoyote katika nyinyi)

Hii inatosha kubainisha upotevu wao .kwa hiyo kutangulia kwa zama hizo hakutoshi kuwa mtu ni katika wema waliotangulia , Imam Muslim ametaja (mwanzo wa swahih)kutokana na Aliy bni Shaqiq Allah amrehemu amesema (nilimskia Abdallah bni mubarak akisema mbele

ya watu : wacheni hadithi ya amr bni thabit kwani alikuwa akiwatukana salaf)

Tumejua kwa yaliyotangulia kuwa maana ya salaf katika istilahi , ni maswahaba , taabiin , na waliowafuatia maswahaba kwa wema mpaka siku ya kiyama, na wakaenda juu ya njia yao ,na kufwata nyayo zao.

NUKTA YA TATU

KUTAJA BAADHI YA MAJINA YA KISHERIA YA WEMA WALIOPITA

Mwenye kuangalia maneno ya wengi katika wenye ilmu atapata kuwa wao wametumia majina mengine, na maana yao ni maana hiyo ya jina tukufu, na haifahamiki kupatikana farka baina ya majina hayo, bali yote yanawafikiana maana zao kabisa , na majina hayo yote yamechukuliwa kutokana na (nususi) maneno yaliyofahamisha hivyo

Ni katika majina hayo;Ahlu ssunnawal jamaa, ahlulhadith,ahlulathar, alfirqatunnajiya, attaifatul mansura , alghurabaa.

Ama kuitwa ahlussunawal jamaa:

Al imam Sufyani Thaury Allah amrehemu amesema : (itakapokufikia khabari kutokana na mtu alioko mashariki mtu wa sunna ,na mwengine yuko magharibi wapelekee salamu, na waombee, ni wachache sana ahlusunnawal jamaa)

Na amesema sheikhul Islam Ahmad bni Abdilhalim bni Taymiyya Alharrany Allah amrehemu katika الاستقامة (na bid'a imekutanishwa na kufarikiana kama sunna ilivyokutanishwa na jamaa , husemwa ahlussunna wal jamaa , kama inavyosemwa ahlul bidaa wal furka)

Na amesema Allah amrehemu katika mahali pengine kama katika المجموع akiwaelezea ahlusunna : wao ni wenye kushikamana na kitabu cha Allah na sunna za mtume wake ﷺ na waliyowafikiana na waliotangulia wa mwanzo katika muhajirina na answari na waliowafuatia kwa wema) mwisho wa maneno yake.

Na amesema tena :
Na madhehebu ya ahlussunna wal jamaa ni ya zamani yanajulikana kabla Allah hajamuumba Abu hanifa ,malik , ashafii ,na Ahmad ,kwani hiyo ni madhehebu ya maswahaba ambao wameipokea kwa mtume wao , na mwenye kukhalifu madhehebu hayo huwa ni mzushi kwa ahlu sunna)

Na ama kuitwa ahlul hadith na ahlul athar:

Jina hilo liko katika maneno ya maulamaa kama imam Ahmad , Bukhary na wengineo .

Amesema Al imam ibnu Taymiyya Allah amrehemu kama katika المجموع madhehebu ya salaf watu wa hadith , na sunna wal jamaa)

Kisha akataja madhehebu yao , akawataja watu wa hadith na sunna wal jamaa.

Na amesema Al imam Abuu Hatim Arrazy Alhafidh: katika alama za watu wa bidaa ni kuwakashifu watu wa athar (hadith)

Na ametoa alkhatib Allah amrehemu katika شرف اصحاب الحديث kwa isnad sahihi kutokana na Ahmad bni sinanil Qattan amesema : hakuna hapa duniani mzushi yoyote isipokua huwachukia watu wa hadithi , mtu akifanya bidaa huvuliwa ladha ya hadithi katika moyo wake)

Na ama kuitwa al firqatu nnajiya na Attaifatul mansura, jina hilo limekuja katika hadithi mashuhuri hadithi ya kufarikiana : (Hakika banuu israel walifarikiana kwa vikundi sabini na moja , na ummati wangu utafarikiana kwa vikundi sabini na mbili vyote vitakua motoni isipokua kimoja , nacho ni aljamaa)

Hii ni hadithi mashuhuri imethibiti ni swahih ,kinyume na mwenye kuifanya dhaifu pia imekuja katika hadithi ya Muawiyya رضي الله عنه iliyotangulia

(لا تزال طائفة من أمتي منصورين على الحق...)

(Hakitawaacha kuendelea kikundi katika umati wangu juu ya haki)

Amesema Alhafidh Allalakaaiy katika sharh usuli itikadi ahli ssunnati wal jamaa (hicho ni kikundi kilicho nusuriwa na ni kikundi kilichookoka na ni

kikundi kilichoongoka na ni kundi adilifu lenye kushikamana na sunna) fikiria Allah akuhifadhi sifa hizi tukufu.

Na amesema sheikhul Islam bni Taymiyya Allah amrehemu katika utangulizi wa العقيدة الواسطية ama baada ya hayo, hii ni itikadi ya kikundi kilichookoka kilicho nusuriwa mpaka qiyama kitakapo simama , watu wa sunna na jamaa

Na amesema shekhe wa mashekhe wetu mwanachuoni Hafidh Hakamy Allah amrehemu katika kitabu chake chenye faida: معارج القبول imekuja hadithi ya mkweli mwenye kusadikishwa (kuwa kikundi kilichookoka ni wale waliokuwa juu mfano wa manhaj alivyokuwa nayo mtume na maswahaba wake)

Ama kuitwa ghurabaa:
Haijifichi kwa mwana sunna hadithi ya ghurabaa iliyo mashuhuri katika swahihi (uislamu ulianza mgeni na utarudi kuwa ni mgeni kama ulivyoanza , pepo ni ya hao wageni)

Amesema imam sufyani Thauriy Allah amrehemu (usianeni kheri Kwa watu wa sunna kwani wao ni wageni)

Na amesema ibnul qayyim Allah amrehemu katika مدارج السالكين akisherehesha hadithi ya ugeni : na waumini ni wageni kwa waislamu na wenye ilmu ni wageni kwa waislamu , na watu wa sunna ambao wanaipambanua sunna na watu wa bidaa ni wageni, na walinganizi wa sunna wenye subra kwa maudhi ya wenye kukhalifu hao walinganizi ni wageni sana ,lakini hawa ndio watu wa Allah kwa haki , hakuna ugeni juu yao, isipokua ugeni wao ni baina ya wengi ambao Allah mtukufu amesema:

﴿وان تطع اكثر من فى الارض يضلوك عن سبيل الله﴾

(Ukiwatii wengi waliopo katika ardhi watakupoteza na njia ya ALLAH) (Surat Al-An’am:116)

NUKTA YA NNE

HUKMU YA KUFWATA NA KUJINASIBISHA NA USALAF

Kila mwislamu anaelekea qibla kwa kuswali kwa ajili ya Allah swala ya faradhi au ya sunna, ni lazima asome suuratil fatiha , na hiyo ni moja katika nguzo za swala ,na ndani yake kuna maneno ya Allah mtukufu:

﴿اهدنا الصراط المستقيم﴾

(tuongoze njia iliyonyooka) (Surat Al-fatiha: 6)

Al imam ibni jariri katika tafsiri ametoa maneno ya Hamza ibni mughira aliposema (nilimuuliza Abul-aaliya kuhusu maneno ya Allah mtukufu (اهدنا الصراط المستقيم) Akasema :ni mtume wa Allah ﷺna maswahaba wake wawili Abubakar na Umar akasema : nikamfwata Alhasan nikamwelezea hayo ? yani nini rai yako? Akasema: amesema kweli na ametoa nasaha)

Unataka Allah akuongoze njia iliyoonyooka zilazimu sunna za mtume wa Allah na zilazimu sunna za maswahaba wake na njia ya maswahaba wake na wa juu wao ni makhalifa waongofu na wa juu wao ni Abubakar na Umar رضي الله عنهم

Na amesema sheikhul Islam ibnul Qayyim katika (بدائع الفوائد) kua uhalisia wa njia hiyo ni kitu kimoja nacho ni : njia ya Allah aliyowawekea waja wake kupitia ndimi za mitume wake na akaijaalia ni yenye kuwafikisha waja wake kwake, na hawana njia ya kufika kwake isipokuwa hiyo, na njia zote zimefungwa isipokua hii nayo ni kumpwekesha Allah na kumpwekesha mtume wake kwa kumtii ,hashirikishwi na kitu chochote katika utumwa wake , na hashirikishwi na mtume wake yoyote katika twaa yake , itakaswe tawhid na itakaswe kumfwata mtume ﷺ , kwa

kuzingatia yaliyotangulia : ni wajibu kufwata njia ya mtume wa Allah ﷺ na njia ya maswahaba wake رضي الله عنهم

Ibnul Qayyim Allah amrehemu ameweka mlango wenye manufaa katika kitabu chake (إعلام الموقعين) kuhusu wajibu wa kuwafwata maswahaba katika salaf , na tutataja baadhi ya dalili hizo:

1. Maneno ya Allah mtukufu

﴿وان جاهداك على أن تشرك بي ما ليس لك به علم فلا تطعهما و صاحبهما فى الدنيا معروفا واتبع سبيل من أناب إلي ثم إلي مرجعكم فأنبئكم بما كنتم تعملون﴾

(Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwat'ii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anaye elekea kwangu. Kisha marejeo yenu ni kwangu Mimi, na Mimi nitakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.) (Surat Luqman:15)

Njia ya kutolea dalili:

Amesema ibnul Qayyim: Kila mmoja katika maswahaba ni mwenye kurejea kwa Allah kwa hiyo ni wajibu kufwata njia yake, maneno yake, vitendo vyake, na itikadi zake ni katika njia yake kubwa.

Na dalili kuwa maswahaba ni wenye kurejea kwa Allah ni kuwa Allah amewaongoza katika uislamu na akasema

﴿ويهدي اليه من ينيب﴾

(na anamuongoza mwenye kurejea kwake) (Surat Ash-Shura:13)

2. Maneno yake mtukufu:

﴿قل هذه سبيلي أدعوا إلى الله على بصيرة أنا ومن اتبعني وسبحان الله و ما أنا من المشركين﴾

(Sema: Hii ndiyo Njia yangu - ninalingania kwa Allah kwa kujua - mimi na wanao nifuata. Na ametakasika Allah! Wala mimi si katika washirikina.) (Surat Yusuf: 108)

Njia ya kutolea dalili kwa aya hiyo: amesema ibnul Qayyim Allah amrehemu: “Allah mtukufu ameelezea kuwa mwenye kumfwata mtume ﷺ hulingania kwa Allah, na anaelingania kwa ALLAH juu ya ilimu: ni lazima kumfwata kwa maneno ya Allah mtukufu aliponukuu maneno ya majini na akayaridhia: akasema

﴿يا قومنا أجيبوا داعي الله وامنوا به﴾

(Enyi jamaa zetu muitikieni mlinganizi wa Allah na mumuamini) (Surat Al-Ahqaf: 31)

Na kwa sababu mwenye kulingania kwa Allah juu ya ujuzi analingania haki hali ya kuijua , na kulingania hukumu za Allah ni kulingania kwa Allah na ni kulingania katika kumtii Allah katika aliyoamrisha na kukataza, hivyo maswahaba رضي الله عنهم walimfwata mtume ﷺ, kwa hiyo ni lazima kuwafwata wakilingania kwa Allah)

3. Maneno ya Allah mtukufu

﴿ومن يعتصم بالله فقد هدي الى صراط مستقيم﴾

(Na mwenye kushikamana na Allah huyo ameongozwa katika njia iliyonyooka) (Surat Aal-E-Imran: 101)

Njia ya kutolea dalili kwa aya hiyo : amesema ibnul qayyim Allah amrehemu Allah mtukufu amewaelezea watu wenye kushikamana nae kuwa wao wameongozwa katika haki , tunasema: maswahaba رضي الله عنهم ni wenye kushikamana na Allah kwa hiyo wao ni wenye kuongozwa hivyo ni lazima kuwafuata)

4. Maneno ya mtume ﷺ

katika hadithi ya Irbaadh ibni Saariya iliyo mashuhuri , katika hadithi hiyo alisema : jilazimisheni kufwata sunna zangu na sunna za makhalifa waongofu wenye kuongozwa , ziumeni kwa meno ya mwisho (magego) na tahadharini mambo yenye kuzushwa, kwani kila uzushi ni upotevu) hii ni hadithi sahihi wameitaja wenye vitabu vya hadithi

Njia ya kutolea dalili : amesema ibnulQayyim mtume ﷺ amekutanisha sunna za makhalifa wake na sunna zake na akaamrisha kuzifuata , kama alivyoamrisha kufwatwa sunna zake , na mtume ﷺ alizidisha kuamrisha sunna hizo mpaka akaamrisha ziumwe kwa magego na hii hukusanya yote waliyo yatolea fatwa na waliyoyaweka kwa umma huu, mwisho wa maneno yake رحمه الله

Na amesema ibnu Qudama katika kitabu (ذم التأويل):

mtume ﷺ ameamrisha kushikamana na sunna za makhalifa wake kama alivyoamrisha kushikamana na sunna zake , na akaelezea kuwa mambo yanayozushwa ni uzushi na ni upotevu , na hayo ni mambo ambayo hakufwatwa mtume ﷺ wala sunna za maswahaba wake)

Amesema tena ibnu Qudama : umethibiti wajibu wa kufwata wema waliopita Allah awarehemu kwa Qurani na sunna na ittifaki ya maulamaa , na mazingatio yanafahamisha hivyo , kwani wema waliotangulia hawaepukani na kuwa ni wenye kupatia au wenye kukosea , wakiwa ni wenye kupatia ni lazima kuwafwata, kwa sababu kufwata ilivyo sawa ni wajibu na ni haramu kufuata makosa katika itikadi, na pia wao wakiwa ni wenye kupatia wanakuwa juu ya njia iliyonyooka , na mwenye kuwakhalifu ni mwenye kufuata njia ya shetani inayoongoza njia ya motoni.

Na Allah ameamrisha kufwata njia yake, na akakataza kufuata isiyokuwa njia hii,

﴿وأن هذا صراطي مستقيما فا تبعوه ولا تتبعوا السبل فتفرق بكم عن سبيله ذلكم وصاكم به لعلكم تتقون﴾

(Na hakika hii ni njia yangu yenye kunyooka ifwateni na msifwate njia nyingne nyingi zisije zikakupotezeni na njia yake, Allah amewausieni hilo ili mpate kuwa wachaji Allah) (Surat Al-An'am: 153)

Na mtu akidai kuwa hao wema waliotangulia ni wenye kukosea atakuwa ni mwenye kuukashifu uislamu wote, kwa sababu ikifaa wao kukosea katika jambo hili itafaa kukosea kwao katika mambo mengine ya uislamu, na inatakikana kutonukuu hadithi walizozinukuu, pia miujiza ya mtume walioipokea isithibitishwe, hapo mapokezi yatabatilika na sharia itaondoka, na haifai mwislamu kusema hivyo wala kuitakidi hivyo.

KUJINASIBISHA NA USALAF

Umekwishajua ewe mwenye kuwafikishwa kwamba ni wajibu kufwata njia ya waumin ambao ni watu wema waliopita, kwa hiyo kujinasibisha nao ni utukufu kwako, amesema Al Imam ibni Taymiyya Allah amrehemu:
(Si aibu kwa mwenye kudhihirisha madhehebu ya salaf na akajinasibisha nayo, bali ni lazima kumkubalia hayo kwa itifaki ya maulamaa kwani madhehebu ya salaf hayawi isipokuwa ni haki.)

Na lau unapofikiria nyasia za maimamu ungepata kuwa wao wanausia kufwata na kulazimu njia ya watu wema waliopita رضي الله عنهم na wamekataza kujiepusha na njia hiyo

Ni katika Nyasia hizo

1. Qauli ya Al imamul Awza3i imamu wa watu wa sham :

(Ivumilie nafsi yako juu ya sunna na simama mahali waliposimama watu, na sema waliyoyasema, na jizuie waliojizuia, na fwata njia ya wema waliopita, kwani yanajuzu kwako yale yalojuzu kwao)

2. Na amesema tena:

(Jilazimishe kufwata athari za salaf hata watu wakikukataa, na tahadhari na maoni ya watu hata wakikupambia maneno yao, kwani mambo yatabainika wakati yatakapobainika, na wewe utakua katika njia iliyonyooka)

3. Na amesema al Imamu Abu Uthman ismail Alswaabuun katika kitabu عقيدة السلف اصحاب الحديث

(na wanamfwata mtume ﷺ na maswahaba wake ambao ni kama nyota, na wanawafwata watu wema waliopita ambao ni viongozi wa dini na maulamaa wa waislamu, na wanashikamana na manhaj waliokuwa nayo hali ya kushikamana na dini madhubuti, na haki iliyowazi.)

NUKTA YA TANO

FADHILA ZA KUFWATA SALAF NA USALAF

Mwenye kujilazimisha usalaf wa haki yani njia ya salaf ya haki na ukweli, atapata kheri zote, na atapata thawabu kubwa nyingi; kwa sababu amelazimiana na mwongozo wa mtume wa Allah ﷺ, na katika fadhila hizo:

1- Ni kwamba mwenye kujilazimisha na usalaf ni mwenye kufwata amri ya Allah, na hili ni katika mambo anayoyapenda na kuyaridhia : kwani ibadah : ni jina linalokusanya kila analolipenda Allah na kuliridhia katika maneno na vitendo vya Dhahiri na vya ndani , na kuzingatia hilo : mwenye kujilazimisha na amri hizo zilizopita huko nyuma katika wajibu wa kufwata wema waliopita basi yeye ni mwenye kufwata amri za Allah , na mwenye kufwata amri za Allah , Allah humpenda kwasababu amejilazmisha na sharia yake.

2- Ni kwamba mwenye kujilazimisha na usalaf ni mwenye kupata uongofu na kusalimika na upotevu: na hili ni jambo lililowazi na limefahamishwa na hadithi ya Jabir رضي الله عنه katika hadithi ya swahih muslim aliposema mtume صلى الله عليه katika hijatul wadaa ((nimekuachieni kitu ambacho mkishikamana nacho hamtapotea kitabu cha Allah)) na yaliyo katika kitabu cha Allah ni kuamrishwa kumfwata mtume wa Allah ﷺ na kuwafwata wema waliopita kama zilivyopita dalili nyingi katika hayo.

3- Mwenye kujilazimisha na usalaf ni mwenye kuhifadhiwa, na mwenye kusalimika na kuingia katika ikhtilafu inayokashifiwa na mfarakano unaokashifiwa; kwasababu Qurani na hadithi zinaamrisha na kuhimiza umoja na kushikamana juu ya haki na kwa haki na kwa sababu ya haki .

Amesema Allah mtukufu:

﴿واعتصموا بحبل الله جميعا ولا تفرقوا﴾

(Na shikamaneni na Kamba ya Allah nyote na msifarikiane) (Surat Aal- imran: 103)

Na amesema Allah mtukufu

﴿ولا تكونوا من المشركين ﴿ من الذين فرقوا دينهم وكانوا شيعا﴾

(Na msiwe katika washirikina ambao wameifarikisha dini yao wakawa makundi makundi) (Surat Ar-Rum: 31-32)

Na imekuja katika hadithi ya Alirbaadh iliyopita huko nyuma kwamba mtume ﷺ amesema hakika atakaeishi katika nyinyi ataona ikhtilafu nyingi , kama kwamba maswahaba walimwambia: tutajihifadhi vipi ya rasulallah, na vipi tutaokoka? Akajibu: (jilazimisheni kushikamana na sunna zangu na sunna za makhalifa waongofu wenye kuongozwa …) Amesema Al Imamul Baghawy katika kitabu(شرح السنة) akiisherehesha hadithi hiyo ya Al-irbaadh: katika hadithi hiyo kuna ishara ya kudhihiri au kujitokeza bidaa (uzushi), na Allah anajua Zaidi; mtume akaamrisha kulazimiana na sunna zake na sunna za makhalifa waongofu na kushikamana nazo kwa njia madhubuti Zaidi na kujiepusha na yaliyozushwa dhidi ya sunna hizo

4- Kujikomboa na njia za sheytwan : amesema Al Imam Muhammad ibn nasr Al Marwazy katika kitabu (السنة) Amesema Allah mtukufu:

﴿وأن هذا صراطي مستقيما فا تبعوه ولا تتبعوا السبل فتفرق بكم عن سبيله ذلكم وصاكم به لعلكم تتقون﴾

(Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyengine, zisije zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kumcha Allah) (Surat Al-An'am: 153)

Allah ametuelezea kwamba njia yake ni moja tu iliyonyooka, na kwamba kuna njia nyingi zinazomzuia mwenye kuzifwata kumzuia na njia yake iliyonyooka, kisha akatubainishia hilo mtume ﷺ katika sunna zake, kisha akataja hadithi ya Abdullahi ibni masuud na iko katika musnad ya imam Ahmad na ni hadithi swahih (alitupigia mstari mtume wa Allah ﷺ akasema hii ni njia ya Allah , kisha akapiga mistari mingne mingi upande wake wa kulia na wa kushoto kisha akasema hizi ni njia nyingi, katika kila njia moja katika hizi kuna sheytwan anayelingania katika njia hizi, kisha akasoma

﴿وأن هذا صراطي مستقيما فا تبعوه ولا تتبعوا السبل فتفرق بكم عن سبيله ذلكم وصاكم به لعلكم تتقون﴾

Kisha akataja baadhi ya njia za hadithi hii akasema Allah na mtume wake wametutahadharisha na mambo yenye kuzushwa yenye kuzuia kufwata amri za Allah na sunna za mtume wake ﷺ,

Hadithi hii ni Dhahiri kwamba mwenye kujilazimisha na manhaj hii ya mtume atasalimika na kuingia katika mtego wa njia za sheytwan na njia za upotevu wake . na mwenye kuiwacha njia ya waumini ataingia katika Kamba za sheytwani والعياذ بالله

5- Mwenye kujilazimisha na usalaf ana thawabu za atakaemfwata kwa hadithi aliyoitaja Al Imam muslim katika hadithi ya Jarir ibnu Abdillahi رضي الله عنه amesema mtume ﷺ :

{ mwenye kuhuisha katika uislamu sunna nzuri ana thawabu za sunna hiyo, na thawabu za wenye kutekeleza sunna hiyo baada yake, bila kupunguziwa katika thawabu zao kitu chochote}

Hadithi hii inafahamisha waziwazi kuwa mwenye kuhuisha sunna za mtume ﷺ na mwongozo wa maswahaba wake na watu wema katika ummati huu na kulieneza hilo kwa watu, na wakamfwata watu wengine, yeye ana malipo ya wenye kutekeleza bila kupunguziwa malipo yao kitu chochote.

Amesema Alhafidh Annawawy katika sharh muslim: hadithi hii inahimiza kufanya mambo ya kheri na kuhuisha sunna nzuri na kutahadharisha kuzusha mambo ya baatil na mambo mabaya.

NUKTA YA SITA
KUTAJA BAADHI YA SIFA ZA MANHAJ YA SALAF

Imetangulia kwamba usalaf ni njia iliyonyooka mwenye kufwata usalaf ataokoka, na mwenye kuuwacha atapotea والعياذ با لله , kwa hiyo manhaj hii yenye kubarikiwa, na daawa hii yenye kubarikiwa, ina jumla kubwa ya sifa zilizowazi, na sifa hizo kwa ufupi ni alama za daawa na manhaj ya mtume ﷺ na maswahaba wake baada yake, hakuna vyengine . ni katika sifa za manhaj hii au daawa hii ya usalaf :

1-kuhakikisha utumwa kwa ajili ya Allah mtukufu.

2-kuhakikisha kumfwata mtume wa Allah ﷺ.

3-kulazimiana na ufahamu wa watu wema waliopita رضي الله عنهم kwa dalili za kisheria , na kutotoka nje ya ufahamu wao.

4-kutahadhari na kutahadharisha uzushi n a wazushi.

5-kuwa kati na kati baina ya kupetuka mpaka na kufanya uzembe.

6-kuthibiti juu ya haki.

7-kufanya pupa juu ya haki na kwa sababu ya haki.

8-kutupilia mbali mfarakano na ikhtilafu.

9-kufanya pupa juu ya kupata ilmu yenye manufaa na kuieneza baina ya watu na kuwalingania kwenye ilmu pamoja na kusubiri juu ya maudhi katika jambo hilo.

10-utekelezaji wa ilmu.

Na alama hizi zina dalili kwa mwenye kufikiria maneno ya Qurani na hadithi na mwenendo wa mtume ﷺ

Na ni katika dalili zenye kukusanya alama hizo: hadithi tukufu hadithi ya Irbaadh ibni Saariyaa رضي الله عنه iliyopita huko nyuma Zaidi ya mara moja amesema رضي الله عنه:

{وعظنا رسول الله صلى الله عليه وسلم موعظة وجلت منها القلوب وذرفت منها العيون , فقلنا يا رسول الله كأنها موعظة مودعٍ فأوصنا , قال – أوصيكم بتقوى الله عزوجل , والسمع والطاعة وإن تأمر عليك عبد , فإنه من يعش منكم فسيرى اختلافاً كثيراً . فعليكم بسنتي وسنة الخلفاء الراشدين المهديين عضوا عليها بالنواجذ , وإياكم ومحدثات الأمور فإن كل بدعة ضلالة}

{alitupa mawaidha mtume wa Allah ﷺ mawaidha ambayo nyoyo ziliogopa ,na macho yalitoa machozi, tukasema : ewe mtume wa Allah kama kwamba hayo ni mawaidha ya mwenye kuaga basi tuusie, akasema: nakuusieni kumcha Allah na kumsikiliza na kumtii kiongozi hata akiwa kiongozi wako ni mtumwa, kwani atakaeishi katika nyinyi ataona ikhtilafu nyingi: kwa hiyo jilazimisheni na sunna zangu na sunna za makhalifa waongofu wenye kuongozwa, ziumeni sunna hizo kwa magego na tahadharini na mambo yenye kuzushwa, kwani kila uzushi ni upotevu}

Fikiria katika hadithi hii yenye kukusanya faida nyingi zenye kudhihirisha alama za manhaj hii ya kisalaf.

Ndani ya hadithi hii kuna: kuusia kumcha Allah mtukufu na katika kutekeleza hilo kuna kuhakikisha utumwa kwa ajili ya Allah mtukufu ,

Na katika hadithi hii kuna: kuusia na kuamrishwa kulazimiana na sunna za mtume ﷺ na katika kutekeleza hilo kuna kuhakikisha usafi wa kumfwata mtume wa Allah ﷺ

Na katika hadithi kuna: kuusia na kuamrisha na kulazimiana na sunna za makhalifa waongofu na katika kutekeleza hilo kuna kuhakikisha kulazimiana na ufahamu wa watu wema waliopita رضي الله عنهم

Na katika hadithi hii kuna kutahadharisha uzushi na katika kutekeleza hilo kuna kuhakikisha kutahadharisha uzushi na kutahadharisha watu wake

Na katika hadithi hii ni kwamba mwenye kulazimu sunna kwa ufahamu wa watu wema waliopita atahakikisha ukati na kati wa kisheria na uhakika baina ya kupetuka mpaka na uzembe; na atakua kati na kati baina ya vinyume hivyo viwili.

Na katika hadithi hio pia kuna kutahadharisha mfarakano na ikhtilafu unaokashifiwa kwa maneno ya mtume ﷺ

(فسيرى اختلافا كثيرا)

(ataona ikhtilafu nyingi)

Kwa hiyo mwenye kulazimiana na sunna atasalimika na ikhtilafu nyingi.

Na maelekezo hayo ya mtume yanakusanya kwa maneno yake: kuamrisha umoja na kushikamana na haki na juu ya haki na kwa ajili ya haki; kwa maneno yake mtume ﷺ

(فعليكم بسنتي .....عضوا غليها ...)

(Jilazimisheni na sunna zangu na sunna za makhalifa na ziumeni kwa magego.)

Na ni katika jambo linalojulikana wazi kuwa haiwezekani kutekeleza maana hizi na kudhihiri alama hizi isipokuwa kwa ilmu ya kisheria yenye manufaa

Amesema Al Imam ibnu Taymiyya Allah amrehemu kheri na furaha na wema na ukamilifu ni wenye kudhibitika katika sampuli mbili: katika ilmu yenye manufaa na amali njema .

NA KATIKA DALILI YA ALAMA HIZI AU BAADHI YAKE

1- Maneno ya Allah mtukufu akiamrisha kushikamana na kamba yake madhubuti na kutahadharisha kuiwacha

﴿واعتصموا بحبل الله جميعا ولا تفرقوا﴾

(Na shikamaneni na Kamba ya Allah nyote na msifarikiane) (Surat Aal- imran: 103)

2- Na amesema Allah mtukufu:

﴿ وأن هذا صراطي مستقيما فا تبعوه ولا تتبعوا السبل فتفرق بكم عن سبيله ذلكم وصاكم به لعلكم تتقون ﴾

Imetangulia tafsiri yake na ayah ni nyingi katika jambo hilo

3- Maneno ya Allah subhanahu wa taala katika suratul faatiha:

﴿ اهدنا الصراط المستقيم صراط الذين أنعمت عليهم غير المغضوب عليهم ولا الضالين ﴾

(Tuongoze njia ya Allah iliyonyooka njia ya wale ulio waneemesha wasiokuwa wenye kupotea.)

amesema Al Imam ibnul Qayyim Allah amrehemu katika kitabu إغاثة اللهفان njia hii iliyonyooka ambayo Allah ametuusia kuifwata ndio njia aliyokuwa nayo Mtume ﷺna maswahaba wake, na hii ndio njia ya

kati na kati . na iliyo nje ya njia hiyo ni katika njia zenye kupetuka mipaka

4- Maneno ya mtume ﷺ katika swahih muslim:

{إن الله يرضى لكم ثلاثا ويكره لكم ثلاثا فيرضى لكم أن تعبدوه ولا تشركوا به شيئا وأن تعتصموا بحبل الله جميعا ولا تفرقوا فيكره لكم قيل وقال وكثرة السؤال وإضاعة المال}

{Allah anaridhia kwenu mambo matatu na anachukia kwenu mambo matatu: anaridhia kwenu kumpwekesha na kutomshirikisha naye kitu chochote, na kushikamana na Kamba ya Allah nyote na msifarkiane, na anachukia kwenu: mambo ya porojo, na wingi wa maswali, na kupoteza mali ovyo}

Amezidisha Al imam Ahmad katika musnad: na kumnasihi ambae Allah amemtawalisha mambo yenu. Amesema Al Imam ibni Abdulbarri Allah amrehemu katika kitabu التمهيد katika hadithi hii kuna kuhimizwa kushikamana na kamba ya Allah katika hali ya umoja, na kamba ya Allah katika mahali hapa ina kauli mbili:

1- Ni kitabu cha Allah
2- Ni jamaa, na hakuna jamaa isipokuwa kwa kiongozi

Na amesema al imam ibnu Taymiyya Allah amrehemu katika kitabu منهاج السنة akifasiri kamba ya Allah : imefasiriwa kamba yake kuwa ni kitabu chake , dini yake , uislamu na ikhlas na amri zake, na ahadi zake, na twaa yake, na jamaa, na maana hizi zote zimenukuliwa kutokana na maswahaba na wenye kuwafwata wao kwa wema mpaka siku ya malipo, na maana zote hizo ni sahihi: kwani Qurani inaamrisha dini ya uislamu, na hio ndio amri zake na twaa yake , na kushikamana na hivyo vyote inakua katika jamaa, na uhalisia wa dini ya kiislamu ni kumtakasia Allah.

KATIKA ALAMA ZA MANHAJ YA SALAFI NA IMEPITA HUKO NYUMA NI KUTHIBITI JUU YA HAQQ

Amesema Allah mtukufu

﴿يثبت الله الذين امنوا بالقول الثابت في الحيوة الدنيا وفي الاخرة﴾

(Allah anawathibitishia wenye kuamini kwa maneno yenye kuthibiti katika maisha ya duniani na akhera) (Surat Ibrahim: 27)

amesema hudheyfa رضي الله عنه "hakika upotevu haki ya upotevu ni kujua ulilokuwa ukilikanusha, na kukanusha ulilokuwa ukilijua, na tahadhari kubadilika badilika katika dini ya Allah mtukufu; kwani dini ya Allah ni moja"

Na nyote mnajua msimamo wa imam Ahmad Allah marehemu imamu wa watu wa sunna, aliyeudhiwa katika njia ya Allah mtukufu; akadhibiti, Alipigwa viboko na akaadhibiwa katika njia ya Allah na hakuwacha kauli yake ya haki.

Vilevile imam ibni Taymiyya Allah amrehemu aliudhiwa katika njia ya Allah akathibiti kwa hiyo kuthibiti juu ya haki ni katika alama za manhaj hii, na ni katika alama za watu wake wa kweli wenye kuijua haki.

Tunamwomba Allah atupe thabati katika manhaj.

Haya ndiyo niliyokusudia kuyafasiri katika muhadhara huo uliokua mrefu lakini nimeufupisha ili kuwapa nafasi wasomaji kufahamu na kuyarudiarudia yote yaliyomo katika kijitabu hiki.

وصلى الله وسلم وبارك على عبده ورسوله نبينا محمد وعلى آله وأصحابه أجمعين والحمد لله رب العالمين

4/9/2017 **13/12/ 1438**